DARASA LA SHERIA KWA NJIA YA MTANDAO

Sheria ni jambo muhimu sana katika maisha yako. Umuhimu wake unakuja kwa sababu:

1. Kutojua sheria sio kinga dhidi ya kutiwa hatiani. Hivyo ukijifunza sheria utaepuka matatizo mengi.
2. Kuzijua haki zako. Usipozijua haki zako katika masuala mbalimbali hutaweza kuzidai.
3. Kujitetea pale unaposhtakiwa. Ni muhimu sana kujua utetezi unaokubalika kisheria. Maana watu wengi huingia jela au kulipishwa faini au fidia kwa sababu tu ya kutojua utetezi unaokubalika kisheria.

Hivyo basi natangaza darasa la sheria la wiki tano kwa njia ya mtandao kupitia App ya Telegram.

Mambo utakayojifunza ni kama ifuatavyo:

S/N	*MADA*	*YALIYOMO*
1	**SHERIA NI NINI?**	***Maana, historia, na tofauti kati ya jinai na madai.***
2	**VYANZO VYA SHERIA**	***Katiba, Sheria za Bunge, Sheria za Mapokeo, Sheria za Kimataifa, Mila na Utamaduni, Hukumu za Mahakama.***
3	**SHERIA MUHIMU ZA JINAI**	***Kanuni ya adhabu, Mwenendo wa jinai, Sheria ya Ushahidi, na jinsi ya kuvibaini vifungu vya jinai kwenye sheria zingine.***
4	**SHERIA MUHIMU ZA MADAI**	***Madhara, Mkataba, Mwenendo wa madai, Ndoa, Ardhi, na Sheria ya Ajira.***
5	**MAHAKAMA**	***Aina na madaraja Mahakama, ziko wapi na zinafanyaje kazi.***
6	**JINSI YA KUSHINDA KESI MAHAKAMANI**	***Kutathmini kesi, kuandaa nyaraka, na mambo mengine ya kuzingatia mahakamani.***

SIFA ZA KUJIUNGA

Sifa kuu ya kusoma Sheria ya Tanzania ni ujue Kiingereza cha maandishi. Hii ni kwa sababu sheria zetu zote (kasoro Katiba) zimeandikwa kwa Kiingereza. Darasa litaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Na wale ambao Kiingereza ni mgogoro watatafsiriwa maandishi ya Kiingereza.

Sifa ya pili ni uwe unajua kutumia simu-janja na laptop. Kwa kuwa darasa ni kwa njia ya mtandao matirio utayapata kupitia simu-janja na laptop yako.

ADA NI TSHS. 50,000/- TU. KOZI ITACHUKUA WIKI TANO KUKAMILIKA.
UNAWEZA UKALIPA KWA MKUPUO, AU KWA TSHS. 10,000/- KILA WIKI.

Jiunge Kupitia Link Hii. Inahitaji uwe na App ya **Telegram** kwenye simu au laptop yako

https://t.me/joinchat/MG8pGRUMwZs0mkID-mZCYQ

NA KWA UPANDE MWINGINE .....

Kwa kutambua kuwa vyuma vimekaza, na kuna wengine ambao kulipa Tshs. 50,000/- kwa mkupuo au Tshs. 10,000/- kila wiki ni mgogoro – kuna Program ya Maswali na Majibu ya sheria.

Program ya maswali na majibu itakupa idea ya sheria, lakini haitakupika kwa kiwango kama cha darasa kamili la wiki tano.

Program ya Maswali na Majibu ada yake ni Tshs. 3,000/- tu kwa mwezi (yaani ni sawa na Tshs. 100/- tu kwa siku).

KWANINI KUNA MALIPO .... KWA NINI ISIWE BURE TU?

Program hii nimeileta baada ya kuona mapungufu yaliyoko kwenye mitandao mbalimbali hapa Tanzania. Kuna majukwaa mbalimbali ya bure ya sheria mitandaoni lakini yanakwama katika maeneo muhimu matatu:

1. Hayatoi elimu kamili
2. Maswali huwa hayajibiwi kabisa
3. Pale maswali yanapojibiwa huwa yanajibiwa juu juu, au hayajibiwi kwa wakati

Na silaumu hayo majukwa kwa sababu ili kujibu maswali ya kisheria inabidi kufanya utafiti wa sheria zinasemaje, na hukumu za marejeo zinasemaje.

Utafiti kama huo sio kazi ndogo kwa kuwa kuna sheria nyingi tayari, na Bunge linatunga sheria mpya kila mwaka. Mahakama pia zinatoa hukumu mpya za marejeo kila mwaka. Kwa hiyo inabidi mtu anayejibu atumie muda na pesa yake ili kuhakikisha anapata jibu lililosheheni.

Ni kutokana na changamoto hizo ndo maana majukwaa ya bure ya sheria yanapwaya.

Kwa hiyo unataka vya bure vipo mtandaoni. Ila kama unataka kilicho bora zaidi karibu kwenye program hii.

Ili kujiunga nasi

1. Pakua app ya Telegram kwenye simu yako
2. Jiunge kwa kubofya kiunganishi (link) ifuatayo

https://t.me/joinchat/MG8pGRUMwZs0mkID-mZCYQ

ANGALIZO

KAMA NIA YAKO SIO KUJIFUNZA, BALI KUJA KULETA UJUAJI USIHANGAIKE KUJIUNGA MAANA UTAFUNGIWA MARA MOJA. WAJUAJI NI WALE AMBAO WAMESHASOMA SHERIA VYUONI LAKINI HAWAPENDI KUONA WATU WENGINE AMBAO HAWANA UWEZO WA KWENDA VYUONI NAO WAKIJUA SHERIA. WAJUAJI TATIZO LAO KUBWA WANADHANI MAHAKAMA IMEUNDWA KWA AJILI YA MAWAKILI TU.